

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA SABA

10 JUNI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA SABA – TAREHE 10 JUNI, 2026

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

554. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha miundombinu ya Masoko ya Mwika na Makuyuni.

555. MHESHIMIWA EDIBILY KAZALA KINYOMA (KASULU VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara kutoka Kata za Asante Nyerere na Kata ya Shughuliba kwa kiwango cha Changarawe.

556. MHESHIMIWA CLAYTON REVOCATUS CHIPANDO (KIGOMA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Shule tatu mpya za Sekondari Jimbo la Kigoma Mjini ikiwemo ya Sayansi, Sanaa na Michezo na Shule ya Wasichana.

557. MHESHIMIWA SHAFFIN AHMEDALI SUMAR (UYUI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara kutoka Malumba - Mabama Center - Mwigelezi kwa kiwango cha lami.

558. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (CHAMAZI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Masista hadi Rufu Nyampombo ili kuondoa kero kwa Wakazi wa Mtaa wa Rufu ambao wanaongezeka kwa kasi.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

559. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini eneo la MDC njia panda ya Machame litaachwa kwa Wafanyabiashara ili waweze kulitumia na kuanzisha Mji Mdogo wa kibiashara.

WIZARA YA FEDHA:

560. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini Serikali itaweka uzio wa Fedha za Mfuko wa Maji ili zisitumike kwenye matumizi mengine ikizingatiwa adha ya maji bado ni kubwa nchini.

WIZARA YA MAJI:

561. MHESHIMIWA ASIA ABDUKARIM HALAMGA (HANANG’):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itajenga Kisima cha Maji katika Kata ya Basodesha.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

562. MHESHIMIWA ZUBERI YAHYA MFAUME (MOROGORO KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga upya Kituo cha Polisi Mtamba kilichobomoka tangu mwaka 2014 na shughuli zake kufanyika katika Ofisi ya Kijiji.

563. MHESHIMIWA SULEIMAN MOHAMED RASHID (MWERA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itakipatia Gari Kituo cha Polisi Mwera ili kiweze kutekeleza majukumu yake kwa urahisi.

WIZARA YA KILIMO:

564. MHESHIMIWA KIZA HUSSEIN MAYEYE (KIGOMA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha Bodi ya zao la Chikichi na Sheria ya zao hili ili kuratibu uzalishaji wake na mnyororo wa thamani.

565. MHESHIMIWA ALAN THOMAS MVANO (KAKONKO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itapeleka Zana za Kilimo katika Wilaya ya Kakonko ili kuongeza tija katika uzalishaji wa Mazao ya Kilimo.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

566. MHESHIMIWA DKT. REGINA CHRISTOPHER MALIMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itatunga Sheria ya kuwalinda Wazawa katika Miradi ya Uvuvi na Vizimba.

WIZARA YA AFYA:

**567. MHESHIMIWA ABDUL-AZIZ MOHAMED ABOOD
(MOROGORO MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itaondoa malipo yasiyo rasmi kwa Wajawazito ikiwemo gharama za vifaa wanapokwenda kujifungua.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE
NA MAKUNDI MAALUM:**

**568. MHESHIMIWA DKT. CATHERINE CANUTE
JOACHIM (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, upi mpango wa Serikali wa kuimarisha malezi na ulinzi wa Watoto na Vijana ili kukabiliana na mmomonyoko wa maadili na mienendo hatarishi.

**DODOMA
10 JUNI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**